## MAHINDI, MAHARAGE YA SOYA, MCHELE YALIYOUZWA KATIKA SOKO LA UGANDA NA KENYA

Kwa mujibu wa takwimu mauzo ya mahindi, mchele, dengu na maharage ya soya katika Soko la Uganda katika kipindi cha miaka mitano (5) iliyopita 2021 hadi 2025 yalipanda kutoka dola za Kimarekani milioni 154 mwaka 2021 hadi kufikia dola za Kimarekani milioni 109 mwaka 2024, wakati mwaka 2025 mauzo yalifikia dola za kimarekani milioni 45.

**Mauzo ya bidhaa katika soko la Uganda thamani kwa Dola za  Kimarekeni Milioni**

| Mwaka | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| Mauzo ya bidhaa | 154 | 108 | 106 | 109 | 45 |

**Chanzo**: TRA, 2025

### Soko la Kenya

Mauzo ya mahindi, mchele, dengu na maharage ya soya katika Soko la Kenya kipindi cha miaka mitano (5) iliyopita 2021 hadi 2025 yalikua dola za Kimarekani milioni 121 mwaka 2021 na dola za Kimarekani milioni 84 mwaka 2024. Wakati mwaka 2025 ilifikia dola za Kimarekani milioni 10.

**Mauzo ya bidhaa katika soko la Kenya thamani kwa Dola za Kimarekani Milioni**

| Mwaka | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| Mauzo ya bidhaa | 121 | 74 | 19 | 84 | 10 |

**Chanzo**: TRA, 2025

### Fursa ya kuongeza mauzo 2026 hadi 2030

Kwa mujibu wa takwimu, Tanzania bado ina fursa ya kuongeza mauzo katika kipindi cha miaka mitano ijayo 2026 hadi 2030 kwenye mazao mahindi, mchele, dengu na maharage ya soya. Aidha, katika soko la Uganda kuna fursa yenye thamani ya dola za Kimarekani milioni 135 wakati Soko la Kenya lina fursa ya kuongeza mauzo zenye thamani ya dola za Kimarekani milioni 82.